**JAMHURI YA MUUNGANO WA WANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anuani ya simu 0754 645 903
Unapojibu tafadhali taja

SHULE YA SEKONDARI MWAKAVUTA,
S.L.P 116,
**MAKETE.**

**KUMB. NA. MSS/JI/VOL.1/98/36.** **10/11/2020**

**NDUGU,**
**______________________________**
**______________________________**

**YAH: KUCHAGULIWA KUINGIA KIDATO CHA KWANZA 2021**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao ____________________________________ amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.

Shule itafunguliwa tarehe ______________ hakikisha mwanao anawahi shuleni ili aanze masomo mara moja

Unatakiwa kutoa taarifa ya hali halisi ya kiafya ya mtoto wako ili aweze kupewa msaada utakaohitajika Fomu maalumu imeambatishwa utatakiwa kumpeleka mwanao kwenye hospitali ya serikali kupimwa ili asipate usumbufu yeye mwenyewe na wenzake shuleni.

Utatakiwa kuonyesha ushirikiano wa hali ya juu na walimu katika maendeleo ya mwanao kitaaluma, pia katika tabia na mwenendo. Uvunjaji wa kanuni na taratibu za shule hautavumiliwa kama vile kumnunulia mwanao simu ya mkononi. Tafadhali soma maelekezo zaidi yaliyoambatishwa na barua hii na uyatekeleze kisha jaza fomu zilizoambatishwa na mwanafunzi aziwasilishe shuleni siku anaporipoti.

**ONYO:**
**Kutokana na sheria ya mahudhurio kwa watoto wetu awali hadi sekondari hakikisha unamleta mwanao kwa wakati. Hatua kali na za kisheria zitachukuliwa kwa mzazi yeyote atakayemtorosha mtoto aliyechaguliwa . Halmashauri ya Makete imeagiza kutekelezwa kwa sheria hii.**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SANDUKU LA POSTA 116**

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE**.
Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza (1) katika shule ya sekondari Mwakavuta ambayo ni shule yenye Hosteli kwa wasichana na kutwa kwa wavulana.

**"ELIMU KWANZA"** Hii ndiyo kauli mbiu (moto ya shule hii, ni matumaini yangu utaitafakari na utaitumia nafasi hii kwa manufaa yako, jamii na manufaa ya Taifa.

1. **SHULE ILIPO**

Shule ipo ndani ya wilaya ya Makete kata ya Iniho yapata 27km kutoka Makete mjini kando ya barabara iendayo Mbeya.

2. **TAREHE YA KUFUNGUA SHULE**

Shule itafunguliwa tarehe _______________ unatakiwa kuripoti tarehe iliyotajwa asubuhi walimu wa zamu na walimu walezi watakuwepo kuwapokea.

**NB: Mzazi unatakiwa kumleta mwanao mwenyewe na si kumwacha peke yake.**

3. **SARE ZA SHULE (WAVULANA)**
   - i) Sweta la rangi kijani kibichi.
   - ii) T-shirt yenye nembo ya shule rangi ya blue inapatikana shuleni kwa shilingi 12,000/=
   - iii) Suruali mbili nyeusi .Suruali iwe na mshono wa turnup, celebration na mifuko mitatu mmoja nyuma na mbele miwili. (kama kitambaa kina utata aje na fedha suruali zinapatikana jirani na shule kwa sh. 20,000)
   - iv) na uje na tai ndefu nyeusi.
   - v) Mashati mawili (2) tetron mikono mirefu yanayoweza kuchomekwa ndani ya suruali uje nayo.
   - vi) Uje na "jazzy" za michezo rangi nyekundu au blue na viatu vya michezo jozi moja. Michezo hapa shuleni ni lazima.

vii) Suruali za khaki (2) mbili suruali moja aivae wakati anakuja kuripoti, jambo la kuzingatia ni kwamba mwanafunzi hatakiwi kuja na nguo za nyumbani za aina yeyote ile (tafadhali zingatia hilo). Suruali iwe na mshono wa turnup, celebration na mifuko mitatu mmoja nyuma na mbele miwili.

viii) Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
ix) Soksi jozi mbili ndefu nyeusi.

x) Track suit 1 ya blue au nyeusi yenye fito nyeupe itavaliwa usiku wakati wa "night preparation".

xi) Jacket 1 zito jeusi lenye kofia lisilo na maandishi yoyote kwa ajili baridi, majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi kabisa.

xii) Gloves nyeusi zisizo na maandishi kwa ajili ya baridi (zitavaliwa mwezi wa 7 na 8)
xiii) Pull neck nyeusi (kaba shingo)

## 4. SARE ZA SHULE (WASICHANA)

1. Sketi 2 zenye marinda ya kumwaga ndefu zinazovuka magoti 10cm kutoka kwenye magoti na suruali 2 zinapatikana hapa shuleni mwanafunzi aje na sh. 80,000/=.
2. Mashati mawili ya tetron yenye mikono mirefu yanayoweza kuchomekwa ndani ya sketi.
3. Magauni mawili rangi ya damu ya mzee na lightblue, moja avae wakati wa kuja.
4. Jazzy za michezo rangi nyekundu au blue na raba za michezo jozi moja. Michezo ni ya lazima.
5. Viatu vya ngozi jozi mbili rangi nyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu.
6. Soksi jozi mbili ndefu nyeupe.
7. Track suit moja ya blue au nyeusi itavaliwa wakati wa usiku nightpreparation.
8. Jacket moja zito jeusi lenye kofia lisilo na maandishi yoyote kwa ajili ya baridi, majaketi marefu yanayovuka magoti hayaruhusiwi kabisa.
9. Gloves nyeusi zisizo na maandishi kwa ajili ya baridi.(zitavaliwa mwezi wa saba na wa nane)
10. Pull neck nyeusi (kabashingo).
11. Tai rangi ya kijani itapatikana hapa shuleni.
12. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na hijabu nyeupe kwa ajili ya kuvaa darasani wakati wa vipindi, damu ya mzee, nyeusi, light blue hizo zitavaliwa na shamba dress.
13. T- sheti yenye nembo ya shule itapatikana shuleni kwa sh. 12,000/=

**MUHIMU**

Shule yetu hairuhusu mwanafunzi kuvaa nguo za nyumbani akiwa hapa shuleni. Nguo zozote za nyumbani zitanyang'anywa na hatarudishiwa. Mpe mahitaji muhimu na si nguo zozote za nyumbani. Nguo za nyumbani atavaa wakati wa likizo nyumbani.

1. Kutokana na baridi kali usiku tumeruhusu mwanafunzi aje na koti 1 zito jeusi ambalo halina maandishi atavaa usiku anapokuwa darasani unaweza kununua gloves zito ambazo atavaa kipindi cha baridi kali.

2. Ni mwiko kabisa mzazi kumpa simu mwanao. Akipatikana nayo adhabu kali itatolewa watatumia simu ya shule kwa mawasiliano na walezi/wazazi wao.

3. **MAHITAJI MENGINE MUHIMU**
   - i) Godoro la futi 2.5 Blanketi zito.
   - ii) Mto, foronya ya blue/pinki na taulo.
   - iii) Ndoo 1 ya lita 10 kwa ajili ya matumizi ya shule.
   - iv) Shuka moja (01) la blue na shuka 1 la pinki
   - v) Vifaa vya usafi (slesha, soft broom na chelae)
   - vi) Vyombo vya chakula, bakuli yenye mfuniko, kijiko na kikombe wanafunzi wote wanakula shuleni ili wasipate usumbufu wa kujipikia na utoro sugu. Fomu ya michango ya chakula imeambatanishwa. Atalipa kwa awamu. Soma fomu hiyo kwa makini. Pia kigaloni cheupe cha lita 5 cha kutunzia maji ya kunywa.
   - vii) Mathematical set (mkebe).
   - viii) Daftari 10 aina ya counter (kuanzia quire 2)
   - ix) School bag 1 imara na si mfuko wa kisalufeti.
   - x) Dictionary ya kiingereza kwenda Kiswahili na Atlas
   - xi) Truck suit blue au nyeusi kwa ajili ya michezo.
   - xii) Nguo za michezo jazzy 1 ya kijani na raba za michezo pair 1 kwa wote. michezo kwa sasa ni lazima kwa wote.
   - xiii) Tranka la kuwekea nguo zake na vitu vyake. Asilete begi laini
   - xiv) Toilet paper za kutosha au mpe fedha za kununulia zitapatikana hapa shuleni suala hili ni lazima shule ina vyoo vya kisasa **haturuhusu** karatasi ngumu.

**MUHIMU**: Mwanafunzi atakaguliwa mara baada ya kuripoti hapa shuleni.

3. **AFYA**

Unatakiwa kupima afya yako kabla ya kuripoti shuleni fomu maalumu imeambatanishwa kwa ajili hiyo na unatakiwa kukabidhi fomu hiyo iliyokamilika mara tu ufikapo shuleni kama una matatizo ya muda mrefu ya kiafya toa taarifa, mzazi usifiche tatizo la mwanao.

I. Kutakuwa na uchunguzi wa mara kwa mara kwa wasichana kuhusu afya zao

II. Pia mwanafunzi hatakiwi kuwa na nywele ndefu salooni ipo atanyolewa na kuwa msafi na mwenye afya nzuri. Atanyolewa kwa sh. 500/= tu.

**NB: Suala la chakula ni agizo la serikali linalotakiwa kutekelezwa**

4. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI.**
   - a. Wizi.
   - b. Uasherati, ubakaji na ushoga
   - c. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
   - d. Uvutaji wa bangi
   - e. Makosa ya jinai

f. Kupigana au kupigwa
g. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
   Kudharau bendera ya Taifa
h. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule ni kifungo cha miaka 3 bila faini
i. Kutoa mimba.
j. Kugoma, kuchochea na kuongoza kuvuruga amani
k. Kutembelea majumba ya starehe na guest houses au hosteli
l. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa.Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzie, waleezi na wakubwa.
m. Kumiliki simu ya mkononi, au laini ya simu ni mwiko kwa mwanafunzi. Kosa hili litasababisha kufutwa shule.
n. Utoro ni kosa kubwa kutoroka au kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali.
o. Ni kosa kwa mwanafunzi kuharibu mali ya shule kama vitabu, madawati, vitanda n.k

**MWISHO**

Mwanafunzi atakapofika hapa shuleni atakaguliwa vifaa vyote vya shule alivyoagizwa kuja navyo mzazi/mlezi jitahidi kumkamilishia mwanao kila kitu.

**Mawasiliano ya shule.**

A. i) Sanduku la Barua S.L.P 116, Makete.
   ii) Simu ya shule hutumika muda wa kazi tu saa 1:30 hadi saa 9:30.
   iii) Namba ya simu ya shule kwa wanafunzi ni 0754 – 645 903

**Usitumie simu za walimu ni kosa shule haitaki kesi na wazazi.**

B. Simu za binafsi za waandamizi walimu ni kama ifuatavyo:-
   i. Mkuu wa shule - 0754 645 903
   ii. Makamu Mkuu wa shule - 0762 141 802
   iii. Mlezi wa wasichana (Matron) 0763 495 630
   iv. Mwalimu wa malezi - 0762 144 240
   v. Mkusanyaji wa chakula - 0762 666 014
   vi. Mlezi wa wavulana

Nawatakia kheri katika kutimiza wajibu wenu.

**KARIBU SANA.**

**LUKA N. MKAKATU**
**MKUU WA SHULE.**

**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**
**KAMATI YA WAZAZI SHULE YA SEKONDARI MWAKAVUTA**
**S.L.P 116, MAKETE.**

**MCHANGO WA CHAKULA KWA WANAFUNZI KIDATO CHA I-IV (KWANZA HADI CHA NNE) 2021.**

A. **Nafaka (kwa mwaka**)

- Mahindi debe 8 x 8000 = 64,000/=
- Maharage debe 3@ 25,000/= jumla 3x25000 = 75,000/=
- Mchele debe 1 @ jumla 30,000/=
- Gharama nyingine
  - Kulipa wapishi Tsh. 10,000/=
  - Kununua sukari Tsh. 15,000/=
  - Kukoboa na kusaga Tsh. 16,000/=
  - Mafuta ya kupikia Tsh. 15,000/=
  - Viungo vya kupikia Tshs. 5,000/=
  - Vyombo vya kupikia 5,000/=
  - Nyama Tshs. 6,000/=

  **JUMLA YOTE NI TSHS. 71,000/=**

**JUMLA YA FEDHA YOTE NI 240,000/= KWA WOTE**

**MCHANGANUO WA MCHANGO WA FEDHA NA VYAKULA KWA AWAMU NNE**
**JEDWALI A.**

| AWAMU | WIKI/MWEZI | MAHINDI | MAHARAGE | MCHELE | FEDHA. |
|---|---|---|---|---|---|
| KWANZA | Wiki 1- wiki 4<br>Januari-februari | Debe 2 | KG 15 | KG 05 | 17,750/= |
| PILI | Wiki 1 – wiki 4<br>March – Mei | Debe 2 | KG 15 | KG 05 | 17,750/= |
| TATU | Wiki 1 – wiki 4<br>Julai – septemba | Debe 2 | KG 15 | KG 05 | 17,750/= |
| NNE | Wiki 1 – wiki 4<br>Oktoba – desemba | Debe 2 | KG 15 | KG 05 | 17,750/= |
| JUMLA | Kwa mwaka | Debe 8 | KG 60 | KG 20 | 71,000/= |

**MCHANGO WA FEDHA TU BILA KULETA VYAKULA.**

| AWAMU | WIKI/MWEZI | WASICHANA |
|---|---|---|
| KWANZA | Januari – March | 60,000/= |
| PILI | April – June | 60,000/= |
| TATU | Julai – septemba | 60,000/= |
| NNE | Oktoba - desemba | 60,000/= |
| **JUMLA** | **KWA MWAKA** | **240,000/=** |

1. Unaruhusiwa kuleta nafaka kama mchele, mahindi, maharage au fedha, gharama nyingine zote tunapokea fedha tu.

2. Michango hii inaletwa kwa awamu nne tu hivyo kila mchango (kipengele) kigawanywe katika mihula minne (4) tu au vikaletwa vyote kwa awamu moja tu. Kupunguza usumbufu kwa mwanao.

3. Michango yote iletwe mara tu shule inapofungua ukicheleweshaa zaidi ya wiki mbili hela haitapokelewa utaleta nafaka kama inavyoonyesha kwenye jedwali.

**KAMATI YA WAZAZI**